# ZABURI 137

Ee Bwana, wema wako ndio wa milele

*Mtunzi: Gloire VINCENT*




1. Nitakutukuza, ee Bwana, kwa moyo wangu wote,
   kwani umesikia maneno ya kinywa changu.
   Mbele ya malaika nitakuimbia,
   nitaliangukia hekalu lako takatifu.

2. Nitatukuza jina lako,
   kwa ajili ya wema na uaminifu wako.
   Siku nilipokuita ulinisikiliza,
   uliongeza nguvu rohoni mwangu.

3. Bwana yuko juu, lakini anamwangalia mnyonge,
   na mwenye kiburi anamtambua toka mbali.
   Ee Bwana, wema wako ndio wa milele:
   usiache kazi ya mikono yako.

Fait à Bukavu, jeudi 20 Aout 2026